

Masuala Ibuka katika Fasihi: Mfano wa Insha za Kifasihi za *Staffroom Diary* katika Magazeti ya ‘Sunday Nation’ (Kenya) na ‘Citizen’ (Tanzania)

Moses Wamalwa Wasike, Magdaline Wafula na Mosol Kandagor
Chuo Kikuu cha Moi

Ikisiri

Makala za *Staffroom Diary* ambazo huwasilishwa kwa mseto wa Kiingereza na Kiswahili, ni aina ya insha za kifasihi za mienendo ambazo mbali na kutekeleza jukumu la kuburudisha na kujipatia umaarufu mkubwa miongoni mwa wasomaji wa magazeti ya “Sunday Nation” (Kenya) na “Citizen” (Tanzania) hutekeleza jukumu kuu la fasihi ambalo ni kuzindua na kuelimisha jamii kuhusu masuala anuai yanayoikabili. Kwa kuzingatia nadharia za Udenguzi na Uhalisia, makala hya yanabainisha masuala ibuka yanayojumuishwa katika uandishi wa Mwalimu Andrew.

Maneno Muhimu: masuala ibuka, mtazamo-kike, mtafaruku wa kibabe, udenguzi, uhalisia

Utangulizi

Kwa mujibu wa Simala (2016), suala ibuka linaweza kufafanuliwa kuwa jambo ambalo hatujalifikiria, ilhali ni muhimu kulifikiria, ama suala ibuka ni kitu au hali ambayo tunaifahamu lakini inayobadilika. Iwapo suala ibuka halitashugulikiwa kwa wakati ufaao, linaweza kuathiri vibaya maisha ya binadamu. Munn na wenzake (1999) wanaeleza masuala ibuka kuwa mambo chanya au hasi yasiyotambuliwa lakini yenye athari kubwa kwa binadamu au mazingira.

Kwa mujibu wa Wasike (2015), masuala ibuka ni mambo ambayo yamekuwapo au yamechipuka katika jamii na yanaathiri au yatazidi kuathiri jamii kwa kiwango kikubwa. Ni changamoto zilizokuwapo tangu awali lakini zimeanza kuangaziwa kwa dhati kutokana na zinavyoathiri pakubwa, jamii ya sasa.

Kwa ufupi basi, masuala ibuka huhusiana na ujumla wa maisha: siasa, uchumi, utamaduni, mazingira, teknolojia, fedha, afya. Athari ya masuala haya kwa maisha ya binadamu inaweza kuwa nzuri au mbaya kutegemea hali na muktadha wake. Masuala ibuka katika jamii ya sasa ni kama vile tofauti za kijinsia, maadili, mihadarati, haki za kibinadamu, ufisadi, ugaidi, ubaguzi wa kijamii, utandawazi na TEHAMA, mazingira, magonjwa sugu, demokrasia, imani mpya, uhamiaji, lugha na aina za lugha kama vile pijini (Munn na wenzake, 1999; Wasike, 2015; Simala, 2016). Ojaide (2012) anahoji kuwa taaluma ya sanaa hususani fasihi ya Kiafrika, katika siku za hivi karibuni, inadhihirisha ushahidi mkubwa wa mambo ambayo

hapo awali yangalichukuliwa kuwa kando na sanaa. Anasema kuwa mambo hayo ndiyo yanayoelezwa kuwa masuala ibuka; masuala ambayo sasa hivi ndiyo yanayojenga msingi wa maudhui na fani katika tungo za fasihi. Simala (2016) anasema ni jambo la kawaida siku hizi kuona tungo za fasihi ambazo, zimeandikwa kwa kuongozwa na dhana ya uibukaji (masuala ibuka). Makala za *Staffroom Diary* ni makala zinazochukua mwelekeo huu wa kushughulikia masuala yanayoiathiri jamii. Makala hizi ni aina ya insha za kifasihi za mienendo. Insha za mienendo hujishughulisha na kusawiri mienendo, mitindo na itikadi kwa kusudi la kuitanabahisha jamii kuhusu athari za suala au mienendo hiyo kwa mitazamo, mielekeo na maendeleo ya jamii husika.

Kiunzi cha Nadharia

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kama malighafi ili kuelezea maisha na tajriba ya binadamu, hasa kwa namna anavyotangamana na binadamu wenzake katika mazingira yake. Fasihi ina dhima nyingi ikiwamo ya kuchochea hisia za burudani na kustarehesha kupitia kwa maandishi au usimulizi (Wamitila, 2010). Hata hivyo, fasihi kama kioo cha jamii, hulenga kusawiri picha halisi ya maisha ya binadamu, kwa kubainisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Mwanakombo (2007) anasema kuwa fasihi zote lazima ziwe na vitendo vinavyosababisha iwe na uhalisia. Kwa hivyo, msanii hujaribu kujenga ulimwengu mzima ambao unafanana na maisha halisi ya binadamu. Katika upande mwingine, fasihi huweza kushabiki vituko-dhana au ndoto ili kujenga ulimwengu wa kufikirika usiofanana na maisha halisi, lakini unaoweza kukubalika.

Makala haya yamejikita katika nadharia za Udenguzi na Uhalisia. Nadharia ya Udenguzi inatilia mkazo kwenye lugha inayotumiwa katika kazi ya fasihi. Nadharia ya udenguzi iliasisiwa mnamo miaka ya 1960 ikilenga kupinga mitazamo ya lugha kimuundo iliyokuwepo katika karne ya ishirini katika nchi za Kimagharibi. Iliasisiwa huko Ufaransa na Jaques Derrida na kuchangiwa na wengine kama Foucault, Roland Barthes, Jean Baudrillard, Paul de Man, J. Hillis Miller, Jacques Lacan na Barbara Johnston.

Derrida (1976) anasema kwamba udenguzi hujaribu kuchambua matini kwa kuangilia maana zake mbalimbali kwa lengo la kubainisha vile maana hizo zinajiumbua kiwango cha kujipinga zenyewe. Kwa hivyo ikiwa maana hizi zinajiumbua zenyewe na kufikia kiwango cha kujipinga basi kazi ya fasihi imejivunja yenyewe. Aidha, kila usomaji wa kazi ya sanaa ni toleo jipya la kazi hiyo kwani katika kila usomaji, maana mpya huibuka ambayo huenda ikapingana na ile ya awali. Kwa mujibu wa Derrida kila kiashiria huashiriwa na kingine na kuendelea kuashiriana bila kikomo. Hii inamaanisha kwamba hakuna viashiria wala viashiriwa asilia katika matini kwani ni viashiria vya viashiriwa, jambo ambalo linaleta dhana kuwa hakuna matini asilia wala ile ya mwisho. Aidha,

Derrida anasema kuwa kila matini huwa na maana nyingi na usomaji wowote wa matini lazima uzingatie jambo hili.

Nadharia ya Udenguzi ilifaa utafiti huu kwa msingi wa mhimili unaosema kuwa kuna uwezekano kuwa na fasili mbalimbali za matini moja. Mhimili huu ulitufaa katika kufasiri masuala ibuka katika jamii ya kisasa katika makala za *Staffroom Diary* kwa njia nyingi na kutoa maana tofauti na ile mitazamo iliyokuwepo katika jamii hapo awali. Mhimili huu ulitusaidia kufasiri maana mbalimbali kutokana na kadhia za mhusika mkuu Dre na wakaazi wa Mwisho wa Lami katika makala za *Staffroom Diary*. Nadharia ya Udenguzi ina upungufu kwa kutilia mkazo zaidi matini na maneno na kutozingatia muktadha na historia ya mtunzi na jamii lengwa katika kazi za fasihi (Njogu na Chimerah, 1999; Murithi, 2017). Barthes (1977) anadai kwamba mtunzi anapoandika kazi yake, wajibu wake huishia pale na kwa hivyo si muhimu kuzingatia muktadha wake wa kihistoria, kidini, kikabila na kijamii kwa ujumla. Maandishi tu ndiyo muhimu na kama Njogu na Chimerah (1999) na Murithi (2017) wanavyosema, udenguzi ni uhakiki unaojikita katika kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha. Sifa kubwa ya udenguzi ni uzingatifu wa lugha na matini.

Ni machukulio ya watafiti kuwa maana toshelevu ya matini haiwezi kuwepo bila kuzingatia muktadha wa mtunzi ama mazingira ambamo alitungia. Sababu ni kuwa binadamu ni zao la jamii na huathiriwa na mazingira na muktadha wake tangu utotoni kupitia elimu, vyombo vya habari, mifumo ya uzalishaji mali, dini na kadhalika (Murithi, 2017). Kwa vile utafiti wetu unahusu masuala ibuka na jinsi yanasawiriwa katika makala za *Staffroom Diary* katika muktadha wa uhalisia wa jamii ya kisasa, ni muhimu kuzingatia mihimili ya nadharia ya Uhalisia ili kufidia upungufu wa nadharia ya udenguzi.

Nadharia ya Uhalisia ilizuka mnamo miaka ya 1800 kutuhumu Ulimbende ambao ulisawiri mambo kinjozi; fasihi ya kilimbwende ilitunga mambo yasiyoweza kutimia. Walimbwende waliishi ndotoni. Hivyo wanauhalisia hujaribu kusimulia maisha halisi kwa mapana na marefu yake kwa lugha teule, ili kugusa hisia za msomaji au msikilizaji. Gustav Flaubert (1821-1880), Elliot George (1819-1880), Dean Howells (1832-1920) na George Lucaks (1885-1971) ni baadhi ya wataalam wanaohusishwa na nadharia hii. Uhalisia wa maisha yanayvoonekana na kuthibitishwa kwa tajriba, husawiriwa kama yalivyo bila kudunishwa wala kupigwa chuku kwenye fasihi ya aina hii. Msimamo wa wanauhalisia ni kuwa kazi ya fasihi inafaa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli na halisi.

Kwa mizani hii basi, ni machukulio ya makala hii kuwa kadhia zinazosimuliwa katika insha za *Staffroom Diary* ni uhalisia wa maisha ya jamii ya kisasa. Ingawa kazi yenyewe ni ya kubuni, wahusika ambao ni vipaza sauti vya mtunzi wamepuliziwa uhai mathalani wanadamu wa kawaida wanaoishi katika ulimwengu wanaofahamikiwa nao, wasomaji wa makala haya.

Makala za *Staffroom Diary*

Makala za *Staffroom Diary* ni insha za mienendo zinazoegemea upande wa elimu-burudani (Educational-Entertainment) ambayo husaidia hadhira (wasomaji) kujifunza mienendo inayokubalika katika jamii kwa njia chanya kutoka kwa wahusika wa sanaa hii. Elimu-burudani ni dhana iliyofumwa kuelimisha na kubadilisha mitazamo ya jamii kupitia kwa burudani (Buckingham na Scanlon, 2001). Mtindo huu umetumiwa na taasisi, mashirika, vyombo vya habari na waandishi wa fasihi kupitisha ujumbe wenye lengo la kubadilisha maoni na mitazamo kuhusu masuala ya kijamii kama vile mazingira na afya. Katika fasihi, elimu-burudani huwasilishwa kwa njia ya tashtiti. Fasihi kama burudani, hutupa tashtiti kwa kutuchorea wahusika na mazingira yanayosisimua hisia na utumizi wa lugha kisanii. Tashtiti hutumika kujenga kejeli na masuala yanayohusu jamii yetu.

Makala hizi zilianza kuchapishwa mwaka 2009 katika gazeti la *Sunday Nation*, Kenya. Hivi sasa zinachapishwa katika gazeti la *The Citizen*, Tanzania na *The Monitor*, Uganda. Ni masimulizi ya kitashtiti kuhusu maisha ya mwalimu wa shule kiungani, Mwalimu Andrew almaarufu 'Dre', ambaye ni mhusika mkuu. Dre pia anasomea digrii ya ualimu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, mjini Nairobi; hali inayomwezesha kuzungumzia masuala ya mjini na shambani kwa uketo. Masimulizi yanazungukia Mwalimu Dre na mkewe, Fiolina, jumua ya Shule ya Msingi ya Mwisho wa Lami; Mwalimu mkuu, Skastina Majani almaarufu 'Bensouda', walimu wa kike -Madam Nzomo, Madam Mary, Madam Anita, Mrs Atika, Madam Ruth, Madam Sella, Madam Lena, walimu wa kiume -Kuya, Sapphire, Eric, Oscar na Lutta; wazazi wake; muuza pombe (Hitler); Kasisi Elkana pamoja na marafiki zake wa kijijini - Rasto, Alphayo, Rashid, Nyayo na Toclá.

Masuala ibuka katika *Staffroom Diary*

Kadhia za Mwisho wa Lami zinasimuliwa kwa njia inayotuchekesha lakini kutufanya tutambue masuala nyeti katika mazingira yetu ambayo jamii inayafumbia macho. Mwalimu Andrew ametumia vijenzi vya tashtiti kama vile kejeli (sarcasm), kinaya (irony), ucheshi (humour), chuku (hyperbole) na litifati (parody, mockery or spiteful comments) kuwakilisha uzito wa masuala ya kijamii kama vile jinsia, uafisadi, ulevi, dini, mazingira, TEHAMA miongoni mwa mengine. Makala hii inaakisi masuala ibuka ya jinsia, dini, ulevi na nafasi ya lugha ya Kiswahili.

Suala la Jinsia

Huku tukizingatia mahusiano ya uwezo baina ya jinsia ya kiume na kike, yatupasa kutambua kuwa kulenga jinsia moja tu hakutoshi. Lazima tusaili 'mfumo-dume' na 'ubabe' unavyojitokeza katika jamii na asasi zake pamoja na mtazamo-kike (mapambano ya kuondoa unyanyasaji wa mwanamke katika misingi ya kijinsia) ili kusawazisha mahusiano ya kijinsia na kukadiria matokeo yake. Yatupasa

kuzingatia uhusiano baina ya sauti za kike na za kiume kisha tubainishe msimamo wa mwandishi kuhusu uana.

Mkabala wa kuumeni umetawala jamii nyingi za kilimwengu kwa muda mrefu. Kauli za kidini na kitamaduni zimetumiwa kushadidi uwezo wa wanaume na kuwadunisha wanawake. Kulingana na Beauvoir (1949), jamii asilia ilikuwa na uthamini sawa wa kazi za wanawake na wanaume. Udhalimu dhidi ya wanawake ulianza wakati wa mabadiliko ya ustaarabu yaliyogawa majukumu na kuanzisha urithi upande wa baba. Kazi za wanaume; uwindaji na ufugaji, zilianza kuleta faida zaidi kuliko kazi za wanawake; kazi za nyumbani. Ongezeko la mali upande wa baba lilizusha kuwapo kwa mali ya kibinafsi na hivyo wanawake wakaanza kuwategemea wanaume kiuchumi. Hivi, mwanamume akapata nguvu dhidi ya mwanamke katika nyanja zote kimaisha; kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kimajukumu, mwanamke akawa kwenye nafasi ya pili baada ya mwanamume. Kwa muda mrefu, mwanamke akatengewa mazingira ya jikoni, kuelemezwa mzigo wa kuzaa na kulea, kuhiniwa elimu, na kunyimwa usemi katika vikao vya ‘mabwana’ eti mwanamke ni ‘kitwana’; yupo kuonekenwa wala si kusikika.

Mfumo-dume unaompembeza na kumtelekeza mwanamke umevyaa mvuvumko wa mtazamo-kike ulimwenguni kote wa kumkomboa mwanamke (Momanyi 1998). Zipo juhudi za kumwezesha mwanamke kwa kukuza ukakamavu, ujasiri na nafasi yake kwa kumwondolea mikatale ya kasumba hasi za tangu jadi zinazomdunisha. Hali hii imezua mtafaruku (crisis) kwa upande wa wanaume. Wanachukulia kuwa nafasi yao kileleni katika jamii imetishiwa (Kipyegon, 2013). Mwandishi wa *Staffroom Diary* amefaulu kuonyesha mtafaruku wa kimajukumu kati ya wanawake na wanaume katika jamii ya kisasa. Katika makala za *Staffroom Diary*, mwanamke ameubirua nje-ndani mfumo-dume unaomdunisha na kumdhalilisha.

Kipyegon (2013) anasema kuwa katika jamii ya mfumo-dume, maamuzi ya familia, jamii na maisha kwa jumla ni shughuli za mwanamume. Aghalabu mwanamke hashirikishwi katika maamuzi hata kama masuala hayo yanamhusu lakini hulazimika kuitikia maamuzi ya mwanamume. Kipyegon (2013) anadai kuwa katika karne ya ishirini, hali hii ilidumishwa kwa kuhakikisha kuwa mwanamke hapewi elimu - akipewa ni ya kiwango cha chini kuliko apewayo mwanamume - itakayomfanya atambue haki zake na kujiinua kiuchumi na kuacha kumtegemea mwanamume. Hata hivyo, hali hii imebadilika katika karne ya ishirini na moja ambapo wanawake wana nafasi sawa kielimu ikilinganishwa na wanaume.

Katika *Staffroom Diary*, Dre anashikilia mtazamo uliopitwa na wakati kuhusu elimu ya jinsia ya kike. Anaona kumwelimisha mwanamke (Fiolina) ni kuzisoza pesa zake. Anasema, “...kufanya hivyo ni kama kuuza ng’ombe kupeleka ng’ombe mwingine shuleni.” (“These are my resolutions for 2016, so help me God” **Sunday Nation, Januari 3, 2016**). Hata hivyo, wahusika wa kike wamejikusuru kupata elimu na kudengua hali hii. Shule ya Msingi ya Mwisho wa Lami ina walimu tisa wa kike, ikilinganishwa na wanaume sita. Hawa ni Fiolina, ‘Bensouda’, Madam

Nzomo, Madam Mary, Madam Anita, Mrs Atika, Madam Ruth, Madam Sella, Madam Lena. Walimu wa kiume ni Dre, Kuya, Sapphire, Eric, Oscar na Lutta. Shule ya kibinafsi ya Sharp Shooters aliyohamia Fiolina, Dre anasema, “...nilishtuka kugundua kuwa wengi wao (walimu) ni wanawake”. (“I am moving in with Fiolina” **Sunday Nation, Mei 7, 2017**). Kauli hii imetumiwa na mwandishi kuonyesha mageuzi ya kijinsia katika uwanja wa elimu, uongozi na uchumi. Imetumiwa kimakusudi kudhihirisha upotovu ulio katika mawazo ya Dre yaliyopitwa na wakati kuwa kumwelimisha mwanamke si muhimu; ni kuharibu fedha. Uhalisia kwa sasa ni kwamba wanawake wana nafasi sawa kielimu na kiuongozi kwani usimamizi wa taasisi za kazi umetwaliwa na wanawake; wanawake ambao wameelimika. Mathalani, usimamizi wa shule ya Mwisho wa Lami unabadilishanwa kati ya walimu wakuu wa kike tu. Bensouda anaposimamishwa kazi, Catherine anapewa cheo hiki. Baadaye Bensouda anarejeshewa mamlaka hayo (“Bensouda’s return dims my hope to be principal” **Sunday Nation, Januari 28, 2018**).

Isitoshe, wanawake wanapopewa majukumu ya uongozi wanaonekana kuyatekeleza vyema kuliko wanaume. Uchapakazi wa Skastina Majani (Bensouda) kama mwalimu mkuu wa Mwisho wa Lami, unadhihirika kupitia matokeo ya mitihani ya K.C.P.E. yaliyoimarika tangu ujio wake (Why Bensouda is the best HM” **Sunday Nation, Machi 27, 2016**). Uchapakazi na uthabiti wa wanawake kiuongozi unadhihirika katika lakabu wanazopewa wanawake viongozi katika makala za Staffroom Diary; Skastina Majani na Olive Mugenda. Kutokana na ushurutishi na kutotikisika kwake kimsimamo, Skastina anapewa jina ‘Bensouda’; jina la mwendesha mashtaka wa kike na shupavu wa korti ya ICC nchini Uholanzi wakati wa kesi za jinai zilizowakabili viongozi wa Kenya kufuatia vurugu za baada ya uchaguzi wa 2007. Mbali na hilo, Dre na jumuiya ya Mwisho wa Lami inamrejelea Skastina kama ‘Female Headmaster’ (hedimasta mwanamke). Aidha, katika makala hizo za *Staffroom Diary*, Dre anamwita Prof. Olive Mugenda, aliyekuwa Naibu Chansela wa Chuo Kikuu cha Kenyatta (anakosomea digrii, Dre), ‘University Headmaster’. Kwa wengi, neno ‘Headmaster’ linazua taswira ya kiongozi mkali asiyetetereka. Neno ‘Master’ linabeba taswira ya ‘udume’ au ‘ubabe’ ndani yake. Ndani ya ‘udume’ na ‘ubabe’ huu kuna ishara za ‘ukakamavu’ na ‘msimamo usiotetereka’. Dre ambaye ni msomi anafahamu fika tofauti kati ya ‘Mistress’ na ‘Master’. Hata hivyo waandishi wa makala hii wanachukulia kuwa analitumia kimakusudi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Udenguzi, hakuna maana moja ya neno ambayo ni toshelevu. Maana ya neno ni mpito. Neno ‘Headmaster’ ni kiwakilishi cha mamlaka makubwa. Ikichukuliwa kwamba hapo awali, wanaume ndio waliopewa elimu na hivyo kupata kazi za kufundisha na kusimamia taasisi za masomo, neno hili lilibeba usawe wa kimaana na ‘ubabe’, ‘mamlaka makubwa’, ‘msimamo usiotetereka’ au ‘amri’. (“These are my resolutions for 2016, so help me God”, **Sunday Nation, Januari 03, 2016**).

Kaifa hizi katika *Staffroom Diary* ni ithibati tosha kukoleza sababu za wanaume kutumia kauli na tamaduni za kibabe-dume kwa muda mrefu kuhakikisha mwanamke hapati elimu. Mhimili wa Nadharia ya Udenguzi unaoelezea kwamba baadhi za maana katika matini huweza kupingana unatumika kuonyesha jinsi ambavyo msimamo wa Dre unavyojijengua. Katika kauli “...*nilishtuka kugundua kuwa wengi wao (walimu) ni wanawake*”. (“I am moving in with Fiolina” **Sunday Nation, Mei 7, 2017**) msomaji anatanabahishwa kuhusu nafasi halisi ya mwanamke wa kisasa (karne ya 21). Kauli inabainisha jinsi Dre anavyobadilika na kurekebisha msimamo wake kuhusu jinsia ya kike kulingana na mpito wa wakati. Elimu imefumbua uwezo na vipaji vya wanawake katika upeo wa uongozi. Kwa mujibu wa Wood (2013), hali hii hapo awali iliwafadhaisha wanaume kuchelea kuondolewa kwenye kileleta cha mamalaka kijamii.

Kwa mujibu wa Wood (2013), elimu imewafanya wanawake wa kisasa (karne ya 21) kufikia kilele cha ufanisi wa kiuchumi bila msaada wa mwanaume. Dre anashtuka anapogundua Bensouda amenunua gari mwenyewe. “...*sidhani linaweza kuwa lake (gari)...lazima ana bwana tajiri mjini...*”, anasema Dre (History made as our school gets first car” **Sunday Nation, Septemba 04, 2016**). Licha ya kuwa ni mwanamke, ndiye wa kwanza kumiliki gari Mwisho wa Lami. Awali umiliki huu ulihusishwa na wanaume tu, tena wa mjini kama vile Pius, kakake Dre. Kawaida, ufanisi upande wa mwanamke huchukuliwa kuwa hauji pasi na mchango wa mwanamume (Wood, 2013). Kauli ya Dre inawakilisha maoni ya Wood kwamba kuna baadhi ya wanaume katika jamii ya kisasa wanaoamini kuwa wanawake hupanda ngazi ya kiuchumi na uongozi kwa mchango wa wanaume. Kulingana na Wood (2013), ni dhana potovu iliyokita katika mfumo wa kibabe-dume kuwa mwanamke hupanda ngazi kiuchumi na kimamlaka kwa kutumia urembo na mwili wake kimapenzi ila si akili na bidii yake. Idili na jitahada za ‘Bensouda’ kufanikiwa katika mazingira ya kibabe-dume ni ishara ya azimio la wanawake kubinua uhafidhina na kuangaza njia mpya ya kukabidhi wanawake usukani kwenye masuala ya kijamii. Hii ndiyo dhamira ya mwandishi wa *Staffroom Diary*.

Elimu vile vile imewazindua wanawake kugundua haki zao. Ni wakakamavu wasiokubali tena kudhalilishwa. Wameshika usukani kushiriki uamuzi katika mambo yanayowahusu. Dre anasema, “*Wanawake waliosoma kama Fiolina...wanaweza kukusimamia, kukusubukua, kukusuta na hata kukukaidi*”. Katika makala ya **Sunday Nation, Agosti 14, 2016**, “*Fiolina pestering me to top up loan to complete house*”, anazidi kusema, “*Fiolina ambaye Mosoriot TTC imenirejeshia (msomi) ni tofauti na yule wa awali (asiyeelimika)...amekuwa mkakamavu na jasiri anayeamua mambo nyumbani na kusisitiza yazingatiwe. Uamuzi wangu siku hizi umebaki kuwa mapendekezo tu...awali mapendekezo yangu yalikuwa ndio uamuzi...siku hizi Fiolina ananiita huku akiniangalia usoni moja kwa moja*. Maoni haya yametumiwa na mtunzi wa makala za *Staffroom Diary* kama kinaya au kweli-kinzani ya uhalisia kuakisi hali ya ubabedume

ambayo imepitwa na wakati. Ni hali inayokinzana na uhalisia katika karne ya 21 ambapo wanaume wengi wanapendelea kuoa wanawake waliojikomboa kielimu, kiuchumi na kimawazo.

Baada ya kukamilisha masomo ya ualimu, Fiolina anakuwa muamuzi wa masuala ya ndoa yake kwa vile yanamwathiri moja kwa moja. Hii ni kinyume na hapo awali ambapo Dre aliamua na kutekeleza mambo kwa mkondo wake bila mchango wa Fiolina. Anamshinikiza Dre kuchukua mkopo akamilishe ujenzi wa nyumba, apunguze ulevi na kumaliza kusomea shahada yake. Mwandishi wa makala ya *Staffroom Diary* anatumia malalamishi ya Dre kuhusu elimu ya Fiolina kimakusudi kama mbinu ya kweli-kinzani, anapoonyesha tija inayotokana na elimu ya Fiolina kwake Dre. Mathalani, anashinikizwa kukamilisha masomo yake hali kadhalika ujenzi wa nyumba yao. Ingawa maoni ya Dre hayawakilishi mawazo ya wanaume wengi wa karne hii ya 21, mtunzi ameyatumia kimakusudi kudhihirisha nafasi ya mwanamke wa kisasa katika jamii, mintarafu ya faida zinazotokana na ukombozi wake kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Mfumo-dume unaomdhalilisha mwanamke pia una misingi yake katika maumbile ya kibayolojia kati ya mwanaume na mwanamke (Mlaga, 2017). Sifa hizi zimeambatanishwa na majukumu au nafasi kisaikolojia katika jamii ya mfumo-dume. Mathalani, sifa za kimsingi za kibayolojia za mwanaume ni kutungisha mimba. Kwa upande wa mwanamke, za kimsingi ni kubeba mimba na kunyonyesha. Kisaikolojia, sifa hizi zimeambatanishwa na ubabe na udhoofu kwa mwanaume na mwanamke mtawalia. Kwa mujibu wa Mlaga (2017), katika mahusiano ya kimapenzi au kingono, majina au vitendo vinavyomrejelea mwanamke kimsingi huambatana na kumsawiri kama kiumbe dhaifu akilinganisha na mwanaume. Humsawiri kama ‘mpokezi wa vitendo’, ‘mtendwa’ wala si ‘mtenzi’ anayeamua na kudhibiti mambo. Majina kama ‘chombo’, ‘anakanyagwa’, ‘analiwa’ ni ishara ambazo ni dhaifu na zenye uhasi ambazo zinamdhalilisha mwanamke. Yeye ‘hakanyagi’ wala ‘hali’; ni ‘dhaifu’ na hivyo yuko pale ‘kutendwa’, ‘kutendewa’ au ‘kupokea’ kutoka kwa mwanamume. Kauli hizi zinamwondoa mwanamke katika uamuzi na udhibiti wa usukani wa masuala anayoshiriki.

Wafeministi wa mkondo wa Kiharakati wanaamini kuwa uwezo wa mwanamke wa kuzaa ndio ambao hutumiwa na mwanamume kumdhalilisha na kumtawala mwili wake. Kwa hivyo mwanamke anafaa kutumia uwezo huu kubadilisha na kudhibiti hali impendeleo. Dre anahusiana na Catherine kimapenzi, anampachika mimba na kumwacha akidhani ‘amemfunga bao’. Dhana hii ya ‘kufunga bao’ inabeba ishara kwamba amemlemaza au amemkwamisha kimaendeleo; amemsitisha kupiga hatua kimaisha. Hii ni lugha inayoonyesha uwezo wa mwanaume juu ya mwanamke. Ingawa mawazo haya huenda yasiwajumuishe wanaume wote wa kisasa, kuna baadhi ambao bado wanachukulia kitendo hicho kama ishara ya mamlaka, udhibiti na uwezo wao juu ya mwanamke.

Miaka kadhaa baadaye Catherine anakuja kuwa kaimu mwalimu mkuu (bosi) wake Dre. (“My plans fail as Brandon’s mother becomes my boss” **Sunday Nation, Januari 29, 2017**). Hili linamshtua Dre. Anaona muhali kufanya kazi chini ya mwanamke ‘aliyemfunga bao’ hapo awali. Mtunzi wa *Staffroom Diary* ametumia kimakusudi mawazo yaliyopitwa na wakati kama ya Dre kuwaonya wanaume wenye mawazo kama yake (iwapo wapo), kuhusu kuchukulia suala la mahusiano ya kimapenzi kama ishara ya ubabe kwa mwanamume na udhaifu kwa mwanamke.

Hata hivyo, wanawake wamepitua hali hii sasa na kuweza kuitumia kutangaza uwezo wao. Wamekuwa wanaharakati kutafuta haki zao wenyewe kwa kutumia ‘udhaifu wao wa kimaumbile’ na kuufanya silaha yao kubwa ya kuwatambulishia nafasi yao katika jamii. Katika “Why we have many pregnancies”, (**Sunday Nation, Juni 11, 2017**), walimu wa kike wameamua kutumia uwezo wao wa kuzaa kupaza sauti dhidi ya udhalimu kazini dhidi yao. Walimu wa kike sita kati ya tisa, wanaamua kuwa wajawazito wakati mmoja ili jumua nzima ya Shule ya Msingi ya Mwisho wa Lami inayomdhalilisha mwanamke itambue umuhimu wao (watakosa huduma zao) wakati watakapoenda likizo ya uzazi pamoja. Catherine (kaimu mwalimu mkuu), licha ya kuwa ni mwanamke mwenza, ndiye anayeongoza wimbi la unyanyasaji dhidi ya wanawake wenzake. Anawachukia na kuwavunjia haki ya wafanyakazi ya kufanya kazi katika hali nzuri na mazingira yenye utulivu. Katika jamii inayoandama mfumo-dume (Mlaga, 2017), hata wanawake wenyewe hatimaye huingia katika mkumbo huu na kuuona kwamba ndio uhalisia. Malezi ya mfumo-dume huwakuza wanawake wakakumbatia, wakakubali na kushiriki ubabe-dume kama ndiyo hali ya kawaida na inayostahili. Catherine ni mfano wa hali hii. Licha ya kuwa mwanamke, anawadhalilisha wanawake wenzake.

Ufahamu wa wanawake wa haki zao umezua mtafaruku kati ya mfumo-dume na mtazamo-kike. Mtafaruku huu umezua taharuki miongoni mwa jinsia ya kiume. Kulingana na Pilcher na Imelda (2004), awali wanaume walijificha chini ya mwavuli wa uhafidhina na kuutumia kama pingamizi dhidi ya kuwepo kwa usawa wa kijinsia. Wanaume sasa wamejikuta katika mtanziko. Wanatanga njia mbili; uhafidhina na usasa. Kwa upande mmoja, wanaume wanachukulia ukombozi wa mwanamke kama tisho kwa nafasi yao kama wadhibiti na watawala wa mifumo yote ya maisha. Kwanza, wanachukulia mwanamke kama mvamizi na mhujumu wao. Millet (1969) anasema mwanamke aliyesoma na kujikomboa kiuchumi anaogopwa sana kwani huyu ni yule ambaye hukalia wanaume.

Hii inaonekana wazi katika makala za *Staffroom Diary*. Hitler, muuzaji wa pombe anayoipenda Dre, anamuusia hivi Dre: “Kuoja mtu aliyesoma ni kitu kizuri...chungu asikukalie.” (“I borrowed cash from my wife and became a laughing stock” **Sunday Nation, Agosti 27, 2016**.) Ingawa si wanaume wote, kuna baadhi wanaoona kwamba wanawake hawadhibitiki sasa kutokana na elimu inayowafumbua macho na kuwakomboa. Hali hii inamsononesha mwanamume anayechukulia kuwa elimu imemfanya mwanamke awe kaidi. Katika “Fiolina

rejects my new rules of engagement to save our marriage” (**Sunday Nation, Septemba 25, 2016**), Dre anataka kumdhibiti Fiolina shuleni wanakofundisha wote. Mtafaruku unazuka Fiolina anapokaidi kanuni hizo. Ushauri anaopata kutoka kwa rafiki zake ni wa kihafidhina. Alphayo anamrai hivi, *“Vijana wa siku hizi you have jokes...why do you want your wife to work like you...kwanza wewe Andrea na mshahara kubwa wacha bibi akae nyumbani.”* Mtunzi ametumia kauli hii kimakusudi kukejeli mawazo ya kihafidhina ya baadhi ya wanaume ambao bado wanachukulia nafasi ya mwanamke kuwa nyumbani. Ukweli ni kwamba, elimu humzindua mwanamke na kumwezesha kijamii, kiuchumi na kisiasa bali sio kuwa mpinzani wa mwanamke’.

Stepien (2017) katika makala “Why we need to stop talking about a masculinity crisis”, anasema kuwa mwanamume kwa kawaida amekuwa akitumia masuala ya ngono kumdhibiti mwanamke. Ni silaha ambayo amekuwa akitumia kuonyesha nguvu, uwezo, udhibiti na utawala wake dhidi ya mwanamke. Ili kuitwa mwanamume kamili, uwezo wa kufanya ngono na wanawake wengi umekuwa kipimo chake. Hali hii imegeuka kuathiri Dre kinyume. Fiolina anapojifungua, kazi zinakuwa nyingi nyumbani na hivyo wanahitaji yaya. Hata hivyo, Fiolina anamchukulia mwanamume kama kisawe cha ukware. Kutokana na imani iliyokita katika jamii kuwa mwanamume hatosheki kimapenzi, Fiolina anasema hamwamini kukaa nyumba moja na yaya kigori wala mpwawe ambaye ni barobaro na hivyo itabidi aajiri ajuzi asiyeweza kutamanika kimwili. Vilevile, hamwamini Dre na walimu vijana wa kike (“Fiolina taking advantage of my willingness to help with the baby” **Sunday Nation, Machi 3, 2018**). Inabidi achungwe na Fiolina na kuajiri yaya ajuzi. Imani iliyochukuliwa kuwa ishara ya udume sasa inadenguliwa na kuwa ishara inayomhasiri mwanamume mwenyewe.

Kwa upande mwingine, mwanamume anajaribu kuukumbatia usasa na kukubali kuwa jinsia ya kike na kiume ni sawa. Dre anawasili nyumbani mapema na kusaidia katika kazi za nyumbani ambazo huchukuliwa kama za kike. Dre anajishughulisha na kazi kama viele; kupiga deki, kupanga nyumba, kupika, kulea mtoto na kumpeleka mkewe kwenye kliniki. Majukumu sasa wanayafanya nusu bin nusu (“Tough going as Fiolina declines househelp” **Sunday Nation, Januari 7, 2018**). Mwanamume anaona anafaa kupongezwa kwa kukumbatia majukumu mapya, yaliyokuwa ya wanawake hapo awali. Hata hivyo, wanawake wanachukulia kuwa hali hii inapaswa kuwa ya kawaida kwa mwanamume kufanya kazi za nyumbani katika enzi wanamoishi. Presha ya mke (Fiolina) ya kumwamrisha ‘kama mtoto’ inayochukuliwa kuwa kujikomboa kwa mwanamke, inamfanya Dre kutelekeza majukumu yake ya nyumbani. Anatomia uhafidhina kujikomboa. Anaanza kwenda ulevini kwa Hitler, kule “wanaume kamili” hukutana kila siku.

Kwa ufupi, mgogoro kati ya usasa na ukale unamkabili mwanamume na kumwacha katika mtafaruku wa kibabe (masculinity crisis). Hajui aelemee wapi.

Mgogoro huu aghalabu unamfanya mwanamume kurejea na kujificha kwenye ukale kuliko usasa. Sababu ni kuwa uhafidhina umekubaliwa zaidi katika jamii ya sasa inayoegemea mfumo-dume na huwa mwavuli wa muda kwa mwanamume anayekwepa uhalisia. Hata hivyo, uhalisi wa mambo unamlazimu kutekeleza majukumu kama mwanamume wa kisasa sako kwa bako na mwanamke wa kisasa.

Pombe na Athari Zake

Unywaji wa pombe ni suala la kihistoria. Pombe imekuwa ikitumika katika jamii nyingi duniani kote toka karne na karne kama kinywaji na kiburudisho. Minghairi ya hayo, pombe imekuwa na madhara mengi kwa binadamu. Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) 2014 kuhusu unywaji wa pombe duniani, inaonyesha takwimu za athari za pombe kiafya, kiuchumi na kijamii. Licha ya ufichuzi huu, jamii inazidi kulifumbia suala hili macho. Jumanne (2016) anazungumzia utukuzaji wa pombe na unywaji wake katika vyombo vya habari. Anataja matangazo ya biashara kuhusu pombe na habari zinazoonyesha ubabe na ulimbwende unaotokana na unywaji pombe kwenye redio, mitandao na televisheni. Anabainisha hasa mchango wa video za muziki zinazosimua hamu ya jamii na kuhlalisha unywaji wa pombe.

Makala za *Staffroom Diary* zinaelekea kuchukua mkondo huu wa kutukuza unywaji pombe na kuyafumbia jicho madhara yake. Mwalimu Andrew anaonyesha kuwa anayekunywa pombe ndiye ‘mwanamume kamili’. Pombe inatumiwa kama kigezo cha kuonyesha na kupimia ubabe wa mwanamume. Katika makala, “*Fiolina taking advantage of my willingness to help with the baby*” (**Sunday Nation, Machi 3, 2018**) Dre anasema, “*All Mwisho wa Lami men worth their name went to Hitler’s every evening*”. Kwa kuchelea asichukuliwe kuwa asiye mwanamume kamili, Dre anajiunga na walevi wenzake mangweni kwa Hitler. Hii ni licha ya kuwa ana majukumu ya malezi yanayohitaji mchango wake nyumbani. Isitoshe, hana hela za kununulia pombe. Anaishia kukopa.

Suala la msongo-rika ndilo linaloongoza miongoni mwa sababu zinazofanya watu kuelemea ulevini (Ripoti ya Shirika la Afya Duniani, 2014). Shinikizo hili limedhihirika katika makala za *Staffroom Diary*. Dre anahofia kuchukuliwa kuwa mwanamume dhaifu asipojiunga na wenzake ulevini. Jumanne (2016) anasema kuwa ingawa walevi wengi hukataa kuwa msongo-rika ndio msukumo katika uraibu wao, wao husingizia shinikizo za ugumu wa maisha unaofanya pombe kuwa liwazo bora. Uhalisia ni kwamba, liwazo hili huwa ni la muda tu. Pombe inapoisha akilini na mhusika kupata urazini, shida bado iko pale. Hivyo, dhana hii ni ya kujidanganya tu. Dre anasingizia ‘kukaliwa na Fiolina’ kuwa sababu yake ya kwenda kulewa. Anasema nyumbani hakukaliki; ni vigumu kuridhisha mwanamke; anakumbushwa makosa na majukumu yake kila wakati licha ya kutokuwa na pesa (“*How Nyayo saved Elkana and my son from drowning*” **Sunday Nation, Aprili 8, 2018**). Anaonyesha kuwa kwa Hitler ndiko kimbilio la wanaume wanaotafuta utulivu na amani kutokana na ‘sarakasi’ za wake zao.

Kinaya ni kuwa utoro huu ni kifumba macho tu kwani hatimaye wanaume hawa hurejea kwao kuyakabili hayo ‘matatizo’ waliyoyakimbia. Inadhihirika basi kuwa, ulevi si suluhu ya changamaoto na matatizo katika maisha. Suluhisho ni kuyatatua moja kwa moja.

Ununuzi wa pombe ni mojawapo ya gharama kubwa katika familia zenye wanywaji wa pombe (Ripoti ya Shirika la Afya Duniani, 2014). Ripoti inatoa mfano wa athari kiuchumi kwa jumla kuwa takriban asilimia 60 ya pato la Waafrika Kusini wanaokunywa vileo lilipotea kutokana na matumizi mabaya ya pombe mwaka 2009. Asilimia hii ilitumika katika starehe zao za vileo. Matokeo ni kuwa familia nyingi zilizama zaidi katika umaskini kutokana na wanywaji kutowajibikia majukumu na mahitaji mengine ya kimsingi ya familia zao. Nyayo, rafikiye Dre, anashinda elfu nane kwenye kamari; siku mbili baadaye hana chochote na haelewi alivyozitumia. Zote ziliishia ulevini (“Only Supreme Court will make me pay” **Sunday Nation, Agosti 26, 2017**). Suala la pombe kufilisisha familia limejitokeza kwenye makala za *Staffroom Diary*. Walimu wengi hawafanyi kazi nyingine yoyote kujiinua kiuchumi shule zinapofungwa, na hivyo ulevi unachukua sehemu kubwa ya mshahara wao mdogo. Wanashinda ulevini kwa Hitler tangu asubuhi hadi usiku mkuu. Hivi pia, wanakuwa na muda kidogo na familia zao na hivyo kukosa mshikamano wa kifamilia; wake na watoto wao. (“Can’t schools reopen? Life at home is just unbearable” **Sunday Nation, Disemba 2, 2017**). Walevi wengi, walimu wakiwamo, wanauza vitu vya nyumbani au kuvileta kwa Hitler wapewe pombe ili kukidhi uraibu wao. Dre, mwalimu mzima anajivunja heshima kwa kuleta kuni kutoka kwake kuzibadilisha ili apewe pombe. Aidha, heshima yake pia imeshuka miongoni mwa walevi wenzake akina yahe kwa kushindwa kumudu pombe nafuu ya kina yahe. Isitoshe, ana deni kubwa kwa Hitler.

Ulevi, mbali na kufilisisha na kushusha heshima, unamfanya mtu kupuuza majukumu yake na kuzua mgogoro wa kimahusiano, unaoweza kuvunja familia zao. Katika makala, “My inability to complete degree and house leaves Fiolina fuming” (**Sunday Nation, Septemba 23, 2016**) ulevi unazua mgogoro kati ya Dre na mkewe, Fiolina. Fiolina anamlalamikia mama mkwe kuhusu Dre, “...*shida yangu ni kukunywa kila siku...we have been quarrelling over two things: completing his degree and completing his house*”. Isitoshe, Dre anashindwa kumpa mkewe haki ya ndoa na kuzua mtafaruku kati yao. Dre na Fiolina wanazozania hili hadi Fiolina anamfukuza kutoka chumba chao cha malazi. Sababu ni kuwa Fiolina ameshindwa kuvumilia harufu ya pombe kutoka kwa mumewe ambaye minghairi ya hayo, amekuwa bwege kitandani (“Why I am not about to buy Fiolina any of the strange food” **Sunday Nation, Machi 31, 2018**).

Mbali na kuhujumu ndoa yake, elimu, ujenzi wa nyumba na mengineyo, ulevi pia umemfanya Dre kumtelekeza mwanawe. Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (2014) inaeleza kuwa ulevi pia huweza kusababisha kutelekezwa kwa watoto, na

uharibifu wa kudumu wa ukuaji kihisia wa mtoto wa mlevi. Dre amemtelekeza mtoto wake, Branton aliyemzaa nje ya ndoa. Amedhoofika kiafya na amekosa mavazi muafaka. Mamake Dre anamkumbusha hivi, “*Kuzaa unajua na kulinda watoto hujui...mwezi ujao usipotoa pesa nitamtuma shuleni (unakofunza) uchi*” (“My mother has perfected the art of arm-twisting me for cash” **Sunday Nation, Machi 13, 2016**).

Hatimaye, pombe huleta utegemezi, kudhoofisha afya na kupunguza nguvu-kazi ya taifa husika (Shirika la Afya Duniani, (2014). Pombe humfanya mtu kuwa sakarani asiyeweza kutekeleza lolote bila kunywa pombe. Ikifikia kiwango hiki, mtu huupa ulevi kipaumbele kuliko mahitaji mengine maishani. Unasababisha kutowajibika kazini na kudhoofika kiafya. Halii hii nayo husababisha kudorora kwa uchumi na hatimaye umaskini. Mathalani, Sapphire, mwalimu mwenza wa Dre anakuja shuleni kwa nadra kutokana na uraibu wake wa pombe. Anashinda ulevini siku nyingi za kazi. Dre anasema kuwa muhula mzima, Sapphire alienda darasani mara mbili tu. (“Why Branton moved to my sister’s place” **Sunday Nation, Septemba 10, 2017**). Halikadhalika, amekuwa mlevi sakarani kiasi cha kutojijali. Pombe imemfanya asitambue umuhimu wa kuoa; anastahabu pombe kuliko ndoa na chakula. Anakunywa hadi anakuwa kwenye koma na kuhatarisha afya na maisha yake (“Sapphire’s ‘resurrection’ stirs Mwisho wa Lami” **Sunday Nation, Oktoba 18, 2015**). Nao wanaume wengi wenye umri na uwezo wa kufanya kazi wakiwemo walimu wanashinda kwa Hitler kuanzia asubuhi hadi usiku na kuharibu nafasi ya kufanya kazi na kujiinua kiuchumi (“Can’t schools reopen? Life at home is just unbearable” **Sunday Nation, Disemba 2, 2017**).

Nafasi ya Dini

Dini ni chombo cha kiitikadi au kiimani ambacho kinafungamanishwa na imani ya kuwapo pepo; mahali ambapo watenda mema tu ndio watakaostahili kuingia. Kwa hivyo dini hunuia kutoa mwongozo wa jinsi binadamu anafaa kuishi ili kutimiza hatima ya kuingia peponi. Njogu na Chimerah (1999) wakifafanua nafasi ya dini katika maisha ya binadamu, wanasema dini inafaa kuwa suluhisho la maisha na inatoa mwangaza juu ya tabia zinazofaa kufuatwa.

Kazi za fasihi husawiri nafasi ya dini katika jamii kwa kumfanya msomaji au msikilizaji wake asaili ikiwa dini ni asasi timilifu kama ambavyo imekuwa ikichukuliwa na wanajamii. Mwandishi wa makala za *Staffroom Diary* anatumia katika safari ya kudadisi wajibu wa dini katika maisha. Kasisi katika makala za *Staffroom Diary* anajitokeza kuwa mtovu mkuu wa maadili; kinyume na anavyofaa kuwa. Dhambi na makosa yanatawala harakati zake zote. Awali ya yote, Kasisi Elkana anaonekana kuenda kinyume na lengo la dini la kumfanya binadamu ‘amkaribie Yule aliye mkubwa zaidi kumshinda mwanadamu mwenyewe’ (Omari na Mvungi, 1981). Ili kutimiza lengo hili, wanaoongoza juhudi za kutanabahisha binadamu wenzao kuhusu kuwapo kwa Mungu, wanafaa kuutukuza uwezo wake kuzidi viumbe vingine vyovyote. Kinaya ni kuwa, Kasisi Elkana anaonekana

kujisifu, kujitapa, kujinaki na kutangaza uwezo wake kivitendo kuliko wa Mungu. Katika makala “Fiolina declines househelp” (**Sunday Nation, Januari 6, 2018**), Elkana anaongoza shukrani kwa kuzaliwa kwa Probox, mtoto wa Dre. Dre anasema maombi hayo yaliishia kuwa majigambo ambapo Elkana anajigamba kuhusu nguvu na uwezo wake kimaombi kuhakikisha mtoto amezaliwa salama.

Suala la kuonyesha ubabe katika masuala ya dini yamekita mizizi hasa mwishoni mwa karne ya ishirini na mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja. Vyombo vya dini vimeishia kupotoka kutokana na lengo kuu la kufinyanga maadili kwa misingi ya imani inayohusika (Nwanganga, 2017). Suala hili limetokana na ‘ubidhaashaji’ na ‘ubiasharishaji’ wa dini. Shitemi (2011) anasema kuwa dhana za ‘ubidhaaishaji’ na ‘ubiasharishaji’ ni tendo la kukigeuza kitu au hali kuwa bidhaa au kukichukulia kitu au hali kama bidhaa ya kuuzwa na kununuliwa yaani bidhaa ya kuzalisha mtaji kibiashara. Mahenge (2011) na Mutiga (2018) wanasema kwamba dhana za ubidhaaishaji na ubiasharishaji zinajikita katika muktadha wa ulimwengu wa sasa wa kiutandawazi na kiliberali mamboleo ambao unaangalia kila kitu kupitia fedha na faida. Ni kuiangalia hali yoyote kama bidhaa ambapo itaweza kuleta fedha na faida.

Ubidhaaishaji na ubiasharishaji umepenyeza hadi kwenye uwanja wa dini (Nwanganga, 2017). Hali hii imesababisha ushindani mkubwa miongoni mwa madhehebu ya kidini kuvutia na kujinyakulia waumini wanochukuliwa kama ‘wateja’. Uteja unatokana na sadaka inayotolewa na waumini hawa. Mahubiri yamechukuliwa kama bidhaa katika soko kwa minajili ya kuuzwa na kujipatia tija. Ushindani baina ya makanisa umesababisha viongozi kusana mbinu anuai za kujikolezea umaarufu na mvuto kwa wateja. Miongoni mwa mbinu hizi za kujipatia tija na wateja wengi ni kufanya miujiza ya uongo na kujipatia majina yanayoonyesha ubabe au uwezo mkubwa ambao aghalabu huwa umepigwa chuku. Kasisi Elkana anajipa yeye na kanisa lake, majina mazito mathalani, “Apostle Overseer Elkana, The Spiritual Superintendent” (Mtume Mwangalizi Elkana, Mrakibu wa Kiroho). Kanisa lake analiita “THOAG” (The Holiest of All Ghosts Tabernacle Assembly) ikitafsiriwa kama “Kanisa la Kongamano la Makao Matakatifu ya Yote”. Mashauo yote haya ni kwa ajili ya kuvutia wateja (waumini) na kupata nafasi katika ulimwengu wa kidini uliojaa ushindani.

Viongozi wanaendeleza ulaghai kwa kudai kuwa baraka anazopokea muumini zinalingana na kima cha sadaka anayoitoa. Katika “We’ll ignore Matiang’I and hold prayers” (**Sunday Nation, Oktoba 15, 2017**), Elkana anawaambia wanafunzi wa Mwisho wa Lami kuwa wakilipa (sadaka) vizuri, wataombewa sawasawa wapite mtihani. Sadaka inayolipwa na wanafunzi inakuwa kidogo sana, hali inayomkasirisha kasisi. Anatangaza kuwa kwa vile hawakulipa vizuri wanafunzi hawatapita vizuri kwani alitoa maombi kulingana na sadaka waliyotoa. Hali hii inadhihirisha jinsi maombi yanavyochukuliwa kama bidhaa ya kuuzwa na viongozi wa kidini. Dini imekuwa kitega uchumi.

Nkwera (1977: ix-xi) katika utangulizi kwenye tamthilia ya *Aliyeonja Pepo* iliyotungwa na Farouk Topan, anasema dini inafaa kusaidia kuondoa migogoro mingi katika jamii inayotokana na tamaa kama vile mapigano, watu kuuana na vitendo vinginevyo vya kifuska. Hata hivyo makasisi wamechukua mkondo tofauti unaochangia migogoro hii. Mathalani, Elkana amekuwa mzinifu kiasi cha kupoteza hadhi yake Mwisho wa Lami. Anasababisha kusukasuka kwa ndoa ya Nyayo. Kasisi huyu anahepa na muumini kwa jina Anindo ambaye ni mkewe Nyayo. Anafanya hivi kwa kisingizio kwamba wanaenda Nairobi kama kanisa kumtwesha Papa Mtakatifu Francis. Hii inadhirika kuwa uongo kwa vile walishuka Nakuru na kukaa huko kwa wiki nzima (“Drama as Apostle goes with Nyayo’s wife to meet pope” **Sunday Nation, Novemba 29, 2015**). Dhana ya dini kuwa mlezi wa maadili ya jamii hapa inadenguliwa kwa vile sasa ni nyenzo ya baadhi ya watu kujinufaisha wao wenyewe.

Mwalimu Andrew (mtunzi) anasaili nafasi ya dini katika jamii. Anaibua maswali kama vile; Ni kwa kiasi gani dini imekuwa nyenzo ya kiutawala? Ni nyenzo inayotumiwa kupumbaza watu wasisaili maovu yaliyoko? Majibu ya maswali haya yanatokana na jinsi mwandishi anasawiri uhusiano wa Dre na Kasisi Elkana. Licha ya kufahamu taksiri za kasisi wake (Elkana), Dre hasiti kwenda kanisani kwa maombi. Mwandishi anatuasa, kukataa dini si suluhisho. Suluhisho ni kuondoa ubinafsi na kusaili imani zinazokuwa kama silisili zinazofunga mawazo yetu na uwezo wa kufikiria kwa njia huria kutatua matatizo yetu. Tusiwe watumwa wa dini.

Nafasi ya Kiswahili

Makala za *Staffroom Diary* huandikwa kwa mtindo wa kuchanganya Kiswahili na Kiingereza. Aghalabu, masimulizi yake huwa katika Kiingereza na dayalojia kati ya wahusika huwa kwa Kiingereza na Kiswahili. Mhariri wa makala haya, Martin Mwangi, anasema kuwa kutumia Kiswahili hasa hufanikisha nia ya mtunzi kusawiri na kutambulisha makala na hali halisia ya jamii ya Afrika Mashariki (Khalayi, 2014). Kiswahili hutumiwa kama ‘lugha ya mwananchi’ ambayo hufikia na kuvutia hadhira pana. Hali hii inaonyesha nafasi ya Kiswahili kama lugha yenye uwezo wa kuwaleta pamoja na kuwahusisha watu wa ngazi zote za maisha katika shughuli za kijamii. Kiswahili ni lugha ambayo inafuta mipaka ya kikabila na kitabaka kinapotumiwa katika mawasiliano.

Aidha, mtunzi ameonyesha nafasi ya Kiswahili katika muktadha wa Afrika Mashariki, mintarafu ya mielekeo ya watumiaji wake. Katika jamii yenye wingi lugha, lugha hupewa hadhi tofauti tofauti. Katika jamii yenye wingi lugha kama ilivyo Afrika Mashariki, mielekeo ya wanajamii kuhusu majukumu yanayohusishwa na lugha mbalimbali huwa tofauti tofauti. Mielekeo hiyo huathiri tabia za wanajamii katika kujifunza na kuitumia lugha husika (Mohochi, 2011). Katika eneo la Afrika Mashariki, Kiswahili kinajikuta katika mazingira ya ushindani mkali kutokana na Kiingereza. Kiingereza kimepewa umbele kihadhi

kuliko Kiswahili. Watu huamini kwamba lugha ya walio wengi - kama vile Kiingereza ambayo ni lugha ya kimataifa - ina hadhi ya juu kijamii na kwa kuitumia, wazungumzaji hupata hadhi ya juu kiuchumi kwa sababu inawawezesha kupata nafasi bora zaidi za kazi na kujinua kimaisha ama wao wenyewe au watoto wao siku za usoni.

Katika *Staffroom Diary*, hali hii imedhihirika kupitia kwa matumizi ya lugha ya wahusika. Kuna wale wasiosoma na hivyo hawafahamu lugha zaidi ya moja. Hawa ni wanakijiji kama vile Alphayo, na Toclamba wanadhihirisha matumizi sahihi ya Kiswahili. Hata hivyo, wale ambao wana kisomo na hivyo, ufahamu wa Kiingereza na Kiswahili aghalabu wanahamisha, kuchanganya msimbo na kufanya makosa ya kimatamshi na kisintaksia kwa maksudi. Katika makala “Folina’s drama filled pregnancy” (**Sunday Nation, Oktoba 21, 2017**), Fiolina na wauguzi katika kliniki, hawa wamesoma ila wanaongea Kiswahili bila kuzingatia matamshi na sarufi sahihi. Mathalani, wauguzi wanamwambia Dre, “*Baba watoto, hakuna shida na bibi wako mtoto bado ako mbali sana.*” Katika “Folina taking advantage of my willingness to help with the baby” (**Sunday Nation, Machi 24, 2018**), wauguzi wanasema “*Nani huyu amebeba mtoto kama gunia ya viazi...wapi mama wa mtoto...huyu mtoto hanyonyi vizuri...bado ako vile alikuwa last month*”. Fiolina anamwambia Dre, “*Jipanguze mwenyewe*”. Hii ni baadhi tu ya mifano ya makosa ya kimatamshi na kisintaksia yaliyozagaa katika makala za *Staffroom Diary*. Japo makosa haya yanadhihirishwa na mwandishi katika makala zake, nia yake si kukidunisha Kiswahili bali kusawiri uhalisia wa matumizi ya Kiswahili miongoni wa wazungumzaji wake nchini Kenya, Afrika Mashariki na kwingineko. Mathalani, athari ya lugha asili za wazungumzaji katika matamshi, msamiati na sintaksia ya Kiswahili ambazo hudhihirika katika ulimwengu wa uhalisia hususan Afrika Mashariki yanabainishwa na mtunzi.

Wazungumzaji wa lugha wanapoiboronga kwa hiari kwa kupuuza misamiati ya lugha hiyo pasi na kujali sarufi wala fonolojia yake, ni wazi kuwa motisha ya kuwasiliana inapewa kipaumbele zaidi kuliko sarufi yake. Watumiaji wengi wa Kiswahili, nchini Kenya, Afrika Mashariki na kwingineko aghalabu hawaoni haja ya kuzingatia sarufi na fonolojia yake, ilmradi mawasiliano yamekamilika. Mwandishi amenuia kuonyesha wasomaji wake kuwa hali hii inatokana na mielekeo na dhana kwamba Kiswahili ni lugha ya watu duni kitaaluma ambao walifikia kuhitimu tu kiwango cha chini cha kisomo. Wengi hukitumia tu kutaka kujihusisha na wenzao kama jamii moja ya Wakenya (Mohochi, 2011). Kwamba Kiswahili kimetengewa jukumu la utambulisho wa kijamii na uzalendo huku Kiingereza kikipewa hadhi ya tabaka la juu. Jambo la kusikitisha na kushtua zaidi ni kuwa kwa muda mrefu baada ya kusanifishwa kwa Kiswahili na kufanywa lugha rasmi katika Katiba ya Kenya ya 2010, bado watumizi wake wanakitweza kwa kukizungumza na kukiandika kimakosa.

Hitimisho

Makala haya yanadhihirisha kuwa msanii (Mwalimu Andrew) anachota maudhui yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka ili kutuonyesha picha kamili ya jamii yetu ya kisasa mintarafu ya unafiki wa kidini, dawa za kulevya na athari zake, nafasi ya mwanamke, nafasi ya mwanamume, nafasi ya lugha ya Kiswahili na kutowajibika kazini.

Kupitia mbinu ya uchanganuzi matini, imebainika jinsi suala la uana limezua utata kati ya jinsi mbili. Wakati mwanamke anajizatiti kujiinua na kujinasua kutokana na mikatale ya unyanyasaji wa mfumo-dume, mwanamume anajikuta katika mtanziko; ama wa kutaka kukumbatia mabadiliko na kukubali majukumu mapya yanayomkweza mwanamke au wakati huo huo kupinga mabadiliko na kuendelea na mfumo-dume unaompa mamlaka juu ya mwanamke. Athari za pombe kiuchumi, kijamii na kiafya yanabainika kupitia kwa migogoro inayozuka katika jamii mintarafu ya kutowajibika nyumbani na kazini, kukosa kutimiza malengo ya maisha na kujitunza. Suala la imani likiwa suala la kibinafsi limeshughulikiwa kwa njia inayoonyesha unafiki wa viongozi wa kidini na jinsi binadamu anavyofaa kuchuja mwenyewe na kuamua kufuata yaliyo mema na kutenga yasiyoafikiana na maadili ya jamii. Mwandishi ameonyesha nafasi ya Kiswahili hasa pale ambapo anaamua kujenga kazi yake kwa kutumia Kiingereza lakini Kiswahili kinatumika katika dayalojia kati ya wahusika ili kudhihirisha uhalisia wa matumizi ya lugha hii Afrika Mashariki na kusawiri masuala nyeti katika jamii.

Makala haya yameangazia baadhi tu ya masuala ibuka kama yanavyowasilishwa kifasihi katika karne ya ishirini na moja. Mjadala wa masuala haya unadhihirisha kuwa mpito wa wakati umeathiri mwonoulimwengu wa wanajamii kuhusu masuala mbalimbali kijamii, kisiasa na kiuchumi. Ili kukabiliana na changamoto zinazoibuka kila uchao, mwanadamu hana budi kukubali kuwa fasili ya masuala anuai katika jamii ya kisasa ni telezi na inahitaji umakini kabla ya kutoa maamuzi maalum.

Marejeleo

- Barthes, R. (1977). *The Death of The Author. Image-Music-Text*. (S. Hearth, Mtaf.). London: Fontana
- Beauvoir, S. (1949). *The Second Sex*. London: Crafton Books.
- Buckingham, D. na Scanlon, M. (2001). Parental Pedagogies: An Analysis of British Edutainment Magazines for Young Children. Katika *Journal of Early Childhood Literacy* uk. 288-299.
- Derrida, J. (1976). *Of Grammatology and Writing and Difference*. (G. Spivak, Mtaf.). Balymore: John Hopkins.
- Horatius (Horace), F. (1975). *The works of Horace*. C. Smart & T. A. Buckley (Ed.). <http://www.Perseus.tufts.edu/hopper/text>

- Jumanne, H. (2016). Wataalam: Tanzania Iwe na Sera Maalum Kudhibiti Matumizi ya Pombe. *Mwananchi News*. Dar es Salaam: mwananchinews.co.tz. Toleo la 16.05.2016.
- Khalayi, R. (2014). *The Use of Humour in Socio-Political Commentary in Mwalimu Andrew's Staffroom Diary*. Digital repository. Thesis (M.A.) University of Nairobi, Kenya.
- Kipyegon, E. (2013). *Nafasi ya Utambulisho wa Mwanamke Katika Natala na Kifo Kisimani*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mahenge, E. (2011). *Kiswahili Bidhaa Adimu: Jiajiri*. (2012). n.p. Dar es Salaam
- Millet, K. (1969). *Sexual Politics*. New York: Doubleday and Company Inc.
- Mlaga, K. W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi: Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Limited.
- Mohochi, S. (2011). Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu Lugha ya Kiswahili. *Swahili Forum* 18:24-36.
- Momanyi, C. (1998). *Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Munn, R.E., Whyte, A. V. T. na Timmerman, P. (1999). "Emerging Environmental Issues for the 21st Century: A Study for GEO-2000". *Environmental Information and Assessment Technical Report UNEP/DEI & EW /TR.99-5*. Nairobi: United Nations Environmental Programme.
- Murithi, J. J. (2017). *Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mutiga, J. (2018). Creative Economies and Commoditization of Mother Languages. Katika: L. Chacha, M. Kandagor, S. Ryanga na J. Maitaria (Wah) *Isimu na Fasihi ya Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Mwanakombo, N. (2007). "Mielekeo Mipya katika Ufundishaji wa Fasihi". Katika *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. K. Njogu (Mh.). Nairobi: Twaweza Communications.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nkwera, F. (1977). *Tamrini za Fasihi Simulizi: Sekondari na Vyuho*. Dar es Salaam: Usiness Printers Limited
- Nwanganga, P. (2017). *Church Commercialization in Nigeria: Implications for Public Relations Practice*. Katika *Journal of Philosophy*. <https://www.redletterchristians.org>
- Ojaide, T. (2012). *African literature: New Approaches*. Durham, North Carolina: Carolina Academic Press.
- Omari, C. K. na Mvungi, M. (Wah.) (1981). *Urithi wa Utamaduni Wetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

- Pilcher, J. na Imelda, W. (2004). *50 Key Concepts in Gender Studies*. Los Angeles: Sage Publication.
- Shitemi, N. (2011). *Kubidhaaisha na Kuwezesha Lugha kama Sarafu ya Kiuchumi na Kijamii: Kielelezo cha Taaluma za Kiswahili na Tafsiri. Mhadhara wa uzinduzi*, Eldoret: Moi University Press.
- Simala, I. (2016). "Fasihi Ibuka ya Kiswahili: Hali na Mustakabali Wake". Katika *Kiswahili na Utandawazi*. L. C. Mwita (mh.). Nairobi: Twaweza Communications.
- Stepien, A. (2017). *Why we Need to Stop Talking About a 'masculinity crisis'*. http://www.tcd.ie/news_events/articles
- Topan, F. M. (1977). *Aliyeonja Pepo*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Wamitila, K.W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi* (Chapa ya tano). Nairobi: Focus Publication.
- Wasike, M. (2015). *Tathmini ya Matumizi ya Nyimbo za Kizazi Kipya Kama Mbinu ya Kufundishia Masuala Ibuka Katika Shule za Upili Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili (isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.
- Wood, J. (2013). *Gendered Media: The Influence of Media on Views of Gender*. <http://www.nyu.edu/classes/jackson/causesofgenderinequality>
- World Health Organization, (2014). *Global Status Report on Alcohol and Health 2014*.

